

# HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W))

MKOA WA RUVUMA

Anwani ya Simu: "NYASA  
COUNCIL"

Ofisini Simu Na: 025 -2952003


Fax Na: 025 -2952005

Nyumbani: 025 -

Barua pepe:-

ps.ded@nyasadc.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:



OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W),

S. L. P. 90,

**MBAMBA-BAY,  
RUVUMA.**

Kumb.Na.NDC/L.60/2/VOL.IV/71

12/06/2019

## TANGAZO


Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa anawatangazia wananchi wote wa ndani na nje ya Wilaya ya Nyasa kwamba Halmashauri inatarajia kuuza viwanja vya matumizi ya makazi na biashara katika mji wa Mbamba bay kata ya Kilosa kitongoji cha Sido, Limbo na Linda karibu na eneo linalojengwa makao makuu ya Wilaya ya Nyasa. Viwanja hivi vina ukubwa wa mita za mraba 560 hadi 4200. Viwanja hivyo vitauzwa kwa mita moja ya mraba kwa Tsh. 1,200/= kwa eneo la Low Density Kilosa Sido; Tsh.3,500/= hadi Tsh.4,000/= kwa viwanja vya Linda-Kilosa na kwa viwanja vilivyopo eneo la Limbo Tsh.1,600/= hadi 1,800/=. Miundombinu ya barabara, maji na umeme imesogezwa kwenye viwanja hivyo.

Fomu za maombi zitatolewa kwa Tsh.20,000/=. Fomu zitakazotolewa ni mia moja (100) tu.

Masharti ya mwombaji;

- i. Awe raia wa Tanzania
- ii. Awe mwenye Akili timamu
- iii. Awe mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea
- iv. Awe na uwezo wa kuendeleza kiwanja

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 27/06/2019. Fomu za maombi zinapatika katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) Nyasa na Tovuti ya Halmashauri. Fomu za maombi zitalipiwa mara baada ya muombaji kufika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) na kuandaliwa *bill*. Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na: 0766 441 202 au 0763 403 226 au 0759 444 082

  
Jimson P. Mhagama

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

